Grace Communion International (GCI)

Maandili Ya Wazee

Wa Kanisa La Grace

Communion

International (GCI)

Maandili Ya Wazee Wa Kanisa La Grace Communion International (GCI)

Utangulizi:

Maandili ya wazee wa kanisa la Grace Communion International yameandaliwa kwa lengo la kuimarisha mwili wa Kristo. Ni ombi letu kuwa maandali haya yatakumbatiwa na kila mtu katika nafasi yake ya uongozi iwe ni katika ushirika au nafasi ya utawala. Lengo letu katika kuandaa nyaraka hii ni iwe hai, ili itusaindie kuyarekebisha maisha yetu kila wakati tukijaribu kuifanya bora zaidi ili kuonyesha mapenzi ya Kristo kwetu ndani ya kanisa.

Maandili hupatia watu misingi ya wanavyofanya maamuzi na jinsi ya kuyatekeleza maamuzi yaliyofanyika. Maamuzi katika maisha ya mkristo huwa yana maandili yanaposimikwa katika neno la Mungu na kuongozwa na Roho Mtakatifu, hii ndio tu njia ya kuelewa mapenzi ya Mungu.

Kama wazee wa kanisa, lazima tukikabidhi kwa neno lake Mungu na turumruhusu Roho Mtakatifu atuongoze katika utekelezaji wa maandili na mwongozo wa maandiko matakatifu. Maisha yetu ya Kikristo lazima yafuate mwongozo wa mafunzo ya Kristo, na maelekezo yaliyo kwenye maandiko chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Agano jipya katika Biblia linatuhitaji sisi kama wazee tuwe wenye sifa njema, maandili na tambia nzuri katika jamii.

Kama viongozi wa kanisa, tunatambua kuwa Yesu Kristo anaishi ndani yetu kupitia kwa Roho Mtakatifu. Tunamuomba atubadilishe ili uhalisi wa kufufuka kwake ushuhudiwe katika mawazo na matendo yetu. Mwongozo wa maandili na utaratibu kwa wazee wa kanisa umeandaliwa ili kushikamana na maisha na shughuli zetu ili kuthihirisha uharisi wa maisha ya Kristo ndani yetu.

Kwa hali hiyo, kama wazee wa kanisa katika mwili Kristo, lazima tujaribu iwezekanavyo kuishi maisha yetu kulingana na mwongozo wa maandili.

Wajibu kwa Mungu:

Kwa kutambua kuwa Kristo ndiye kiongozi wa kanisa, nitalenga kuendesha maisha yangu kwa njia itakayomletea utukufu. Hii ina maana nitalenga:

- Kwa mtumishi wa Mungu mwandilifu
- Kuwa Mwaminifu katika maisha ya kujitoa, kupitia maisha ya kiroho yenye nidhamu, na kutoa huduma kwa wahitaji.
- Kuwa Mwaminifu kwa majukumu na rasilimali iliyowekwa chini ya uangalizi wangu.
- Kukumbali kwajibika kwa matendo yangu yote na kuepuka matendo au kuwa kwenye mazingira ambayo yanaweza kuletea jina la Kristo aibu.
- Kuishi maisha safi ya ndoa.
- Kutekeleza uongozi wa Kristo wa ki utumishi.

Wajibu wa kiongozi kwa wazee wa Kanisa.
Katika ungozi wa ndugu wa Kikristo, viongozi wa wazee wa kanisa wanao wajibu wa kuwapa wazee wakanisa msaada na kuwatunza vizuri ili kufanya kazi yao iwe rahisi. Kwa hali hiyo mimi kama kiongozi wa wazee wa kanisa nitajitahidi ku:

- Kupatikana kwa urahisi na kutoa majibu kwa mahitaji ya wazee wa kanisa.
- Kutoa uongozi wa kiroho, kimawazo na kiutawala unaoeleweka.
- Kwa heshima na kwa uwazi kueleza mzee yeyote wa kanisa kuhusu malalamishi yoyote ambayo nimepokea dhidi yake.
- Kutoa majibu ya masuala yoyote yaliyoletwa kwangu na mzee/wazee wa kanisa kwa muda unaotakiwa.
- Kuchukulia kwa makini na kuhifadhi mambo ya kibinafsi ya mzee yeyote wa kanisa kwa uandilifu na kuweka siri mambo yanayotakiwa kuwa ya siri.
- Kuchukulia kwa makini mahitaji binafsi au mahitaji ya kifamilia ya mzee wa kanisa.
- Kuwa muwazi ninapojibu maswali ya wazee wa kanisa.
- Kujitoa na kuwajibika kueleza utekelezaji wa majukumu yangu.
- Kutoa taarifa yenye muda wakutosha kuhusu mabadiliko, kusimamishwa kazi, mabadiliko ya mashahara na marupurupu ya wazee wa kanisa.

Wajibu wa kiongozi kwa viongozi wa ngazi ya juu.

Kama mzee wa Kanisa la Grace Communion International (GCI), ninao wajibu wa kuwatumikia viongozi wa Kanisa katika makao makku ya Kanisa na pia viongozi wa kiutawala juu yaliowekwa juu yangu. Hii inamaanisha kuwa nitajitoa:

- Kwa uvumilifu na kwa kuomba kusoma maelezo yote ya kidini kutoka makao makuu.
- Kuunga mkono na kutekeleza maamuzi na sera zote vinazotengenezwa na viongozi wa kidini waliowekwa juu yangu. Iwapo kwa sababu moja au nyingine nitapata ugumu nafsini mwangu kutenda lolote ninaloagizwa, nitatoa taarifa kwa wasimamizi walio juu yangu.
- Kushikamana na, na kutafuta msaada kutoka kwa wasimamizi waliowekwa juu yangu, tulio kwenye ngazi moja kiutawala na pia washirika kuhusu taranta yangu ya uongozi na matendo yangu.
- Kuheshimu dini yangu, kuwa mwadilifu hasa kuheshimu mazungumzo kuhusu viongozi wenzangu waliopo na waliotangulia.
- Kuunga mkono na kuenzi nia ya kanisa ulimwengu mzima.

Wajibu kwa familia:

Nitaweka wajibu kwa familia yangu katika nafasi ya juu zaidi katika mipangilio yangu, kihalisia itachukua nafasi ya pili kutoka kwa wajibu wangu kwa Mungu. Kwa hali hiyo nitajitahidi:

- Kiroho, kihisia na pia kimwili kujitoa kwa familia yangu.
- Kuwa mwaminifu kwa mwenzangu wa ndoa.
- Kuwajibika na kujitoa kama mzazi kwa wanangu.

Wajibu kwa ushirika:

Nitaongoza kwa haki na huruma, nitajaribu kuweka sawa nguvu na unyenyekevu katika kila tukio. Kwa hali hiyo nitajitahidi:

- Kutoa mwelekeo unaoeleweka wa kidini na wa kiroho.
- Kuwasaidia washirika kutambua na kuziendeleza taranta zao, pia kuwasaidia viongozi watarajiwa kujiendeleza.
- Kuhubiri mahubiri yenye msingi wa Biblia, mahubiri yanayoendana na mafunzo ya kanisa na yanayoendana na maisha ya washirika.
- Nitajitoa kwa haraka iwezekanavyo kutatua mizoz kati ya washirika. Ninatambua ninatakiwa kuwa na ujasiri, kutekeleza maamuzi kwa njia ya hekima nitakapokutana na upinzani.
- Nitakuwa mwaminifu kwa mambo ya siri, isipokuwa kwa yale nitakayotakiwa kisheria kutoa. Sita sariti imani ya watu kwangu kwa kutoa maelezo binafsi kuwahusu bila wao kujua na kunipa idhini kufanya hivyo.
- Kutenda kwa haki na kutegemewa mahusiano yangu yote na wafanyakazi wa kanisa.
- Kudhamini na kuheshimu mira zote, jinsia na kabila.

Wajibu kwa viongozi wenzangu.

Kama mzee wa Kanisa la Grace Communion International (GCI), ninao wajibu wa kuhusu na kuenzi wenzangu. Nitajitahidi kushirikiana na kushikamana na wenzangu tunapofanya kazi pamoja kuieneza injili ya Kristo katika kanisa. Kwa hali hiyo nitajitahidi:

- Kuwaheshimu wenzangu na sitaongea jambo lolote dhidi yao hadharani na kwa siri na nitawachukulia kama washiriki wenza katika kazi.
- Nitaheshimu mipaka ya kiutawala kati yangu na wenzangu katika maeneo ya majukumu.
- Sitatumia ofisi yangu yam zee wa kanisa kama nafasi ya kushindana au kueneza ubinafsi au kujikweza.
- Nitawatumikia wenzangu kwa busara, umakinifu na kuwaunga mkono hasa kuwapa ushirikiano wa kibinafsi.

Wajibu kwa Mwili mzima wa Kristo.

Wazee na kanisa na washiriki kwa ujumla wao ni sehemu ya mwili mzima wa Kristo. Kwa hali hiyo nitajitahidi:

- Sitashiriki katika kuhamisha wakristo kutoka kwenye ushirika mwingine.
- Kufanya kazi pamoja na viongozi wengine wa Kikristo kueneza na kuimarisha mwili wa Kristo ili kufikisha ujumbe wa ufalme wa Mungu.
- Kuheshimu mwili wa Kristo kwa kutodharirisha au kuvumisha maneno kuhusu ushirika mwingine.

Wajibu kwa jamii:

Ushirika ni sehemu ya jamii iliyotuzingira. Maisha ya kujitoa, yanayoendana na utaratibu mzuri wa jamii ni mfano mwema wa upendo na ushahidi wa injili ya Yesu Kristo. Kwa hali hiyo nitajitahidi:

- Kuwa mwadilifu katika jamii.
- Kukubali majukumu katika huduma kwa jamii, kutambua hii ni sehemu ya huduma yangu kwa jamii na kanisa.
- Kuhimiza washirika kushirika kwenye huduma za jamii.
- Kuheshimu na kufuata sheria zilizowekwa na serikani ambazo hazikinzani na sheria za Mungu.
- Kuhakikisha mambo ya kisiasa haleti utengano katika ushirika.